(f) mahali ilipo ofisi ya makao makuu au ofisi ndogo ya makao makuu ya chama, anwani ya posta ya kila ofisi kwa msingi kwamba, kama ofisi kuu iko Tanzania Bara ofisi ndogo itakuwa Tanzania Zanzibar au kinyume chake katika Fomu PP.5D ikiambatana na nakala iliyohakikiwa ya mkataba wa pango au sehemu ya jengo au uthibitisho wa umiliki wa ardhi ambapo ofisi ya chama ipo;

Baada ya kupokea maombi ya usajili kamili, Msajili atachambua nyaraka zinazothibitisha maombi hayo na anaweza kuelekeza masahihisho au marekebisho ya nyaraka hizo.

Mara baada ya kujiridhisha kwamba maombi ya usajili kamili ya chama cha siasa yamekamilika na yako sahihi kwa mujibu wa Sheria atatoa cheti cha usajili kamili kwa chama hicho.

## HAKI ZA CHAMA CHENYE USAJILI KAMILI NA MASHARTI YA KUTUMIA HAKI HIZO

a. Haki ya kufanya mikutano ya hadhara katika eneo lolote la Jamhuri ya Muungano kwa lengo la kujitangaza au kutafuta wanachama, baada ya kutoa taarifa kwa afisa wa Polisi kiongozi wa eneo husika;
b. Haki ya kupata ulinzi na msaada wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama, kwa lengo la kuwezesha mkutano wa hadhara kufanyika kwa amani na utulivu;
c. Haki ya kuweka mgombea au kufanya kampeni kwa mgombea yoyote katika uchaguzi wa ubunge, Rais au Serikali za Mitaa;
d. Haki ya kushirikiana baada ya kukamilisha masharti yaliyowekwa katika Sheria ya Vyama vya Siasa;
e. Haki ya kumiliki, kutumia na kuweka bendera yake katika maeneo ambayo yameanishwa na Sheria;
f. Haki ya kupata ruzuku endapo kina sifa ya kupata ruzuku kwa mujibu wa Sheria;
g. Haki ya kujieleza kabla ya usajili kamili kufutwa;
h. Haki ya kutofutiwa usajili kamili ndani ya kipindi cha mwaka mmoja kuelekea Uchaguzi Mkuu;
i. Haki ya kuomba Mahakama Kuu ifanye marejeo ya uamuzi wa Msajili wa Vyama vya Siasa kuhusu usajili au kufuta usajili wa chama; na
j. Haki ya kuwa na wawakilishi wawili katika Baraza la Vyama vya Siasa, ambao ni viongozi wa kitaifa.

Ni muhimu kufahamu kwamba, haki ya kufanya mikutano ya hadhara inaratibiwa na Sheria kadhaa, zikiwamo, Sheria ya Vyama vya Siasa Sura ya 258, Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma Saidizi Sura ya 322 na Sheria ya Kuweka Utulivu Nchini Sura ya 385. Kwa mujibu wa Sheria hizo, Jeshi la Polisi lina mamlaka ya kisheria kuzuia chama cha siasa kisifanye mkutano wa hadhara au maandamano, kwa lengo la kudumisha amani na utulivu nchini.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU - SERA, BUNGE, URATIBU NA WENYE ULEMAVU
OFISI YA MSAJILI WA VYAMA VYA SIASA

# MCHAKATO WA KUSAJILI CHAMA KIPYA CHA SIASA

## MCHAKATO WA KUSAJILI CHAMA KIPYA CHA SIASA

Moja ya jukumu la msingi la Msajili wa Vyama vya Siasa ni kusajili vyama vya siasa, jukumu hilo linaelezwa katika Kifungu cha 4(4) cha Sheria ya Vyama vya Siasa Sura 258 Marejeo ya 2023. Usajili hufanywa kwa hatua mbili, hatua ya kwanza ni usajili wa muda na ya pili ni usajili wa kamili

1. MAOMBI YA USAJILI WA MUDA

i. Waanzilishi wawili ambao ni raia wa kuzaliwa na ambao wazazi wao pia ni raia wa Tanzania watawasilisha maombi ya kusajili chama kipya kwa Msajili wa Vyama vya Siasa kwa kujaza Fomu PP1. Maombi hayo yataambatana na nyaraka zifuatazo:

   a. Tamko litakalo tolewa kwa kujaza Fomu PP.2;
   b. Nakala mbili za Katiba na Kanuni zilizosainiwa na waanzilishi wawili, zikiwa katika nakala ngumu (hard copy) na laini (soft copy);
   c. Sera pamoja na Itikadi ya chama;
   d. Wasifu wa waanzilishi wawili wa chama hicho;
   e. Vyeti vya kuzaliwa vya waanzilishi pamoja na uthibitisho wa uraia wao na wa wazazi wao;
   f. Picha mbili ndogo za waanzilishi;
   g. Sampuli ya bendera ya chama katika kitambaa na karatasi ya A4; na
   h. Uthibitisho wa malipo ya ada ambayo ni Shilingi milioni moja.

Baada ya Msajili kupokea maombi ya usajili wa muda atafanya yafuatayo:-

(i) Atatoa tangazo angalau kwenye magazeti mawili ambayo yanafika nchi nzima, moja likiwa la Kiswahili na lingine la Kiingereza, akikaribisha pingamizi kutoka kwa mtu yeyote au chama kingine chochote kuhusu jina alama au rangi ya chama kinachoomba usajili wa muda au suala lingine lolote linalohusu usajili wa chama cha siasa husika;

(ii) Atachambua nyaraka zilizoambatana na maombi ya usajili wa muda na anaweza kuelekeza zifanyiwe masahihisho au marekebisho.

(iii) Atatoa cheti cha usajili wa muda baada ya kujiridhisha kwamba, masharti ya sheria yamezingatiwa.

Aidha, hakuna chama cha siasa kitakachokuwa na sifa ya kupata usajili wa muda ikiwa, kwa Katiba, Kanuni na Sera yake au vitendo vyake-

(a) kinakusudia kuhamasisha au kupigania maslahi ya-

(i) imani yoyote ya kidini au kikundi;

(ii) kabila lolote, asili ya jamii au kundi la kimbari; au

(iii) eneo maalum ndani ya sehemu yeyote ya Jamhuri ya Muungano;

(b) kinahamasisha kuvunja umoja unaounda Jamhuri ya Muungano;

(c) kinakubali au kinahamasisha matumizi ya nguvu au vurugu kama njia ya kufikia malengo ya kisiasa;

(d) kinahamasisha au kinakusudia kuendesha shughuli zake za kisiasa katika sehemu moja tu ya Jamhuri ya Muungano; au

(e) hakiruhusu uchaguzi wa vipindi na wa kidemokrasia wa uongozi wake;

(f) kinaruhusu viongozi na wanachama wake kutamka au kutumia lugha chafu, visasi, kashfa au maneno ya uchochezi ambayo yanaweza kusababisha au kushawishi uvunjifu wa amani.

Chama kikishapata usajili wa muda kitakuwa na haki ya kuzunguka nchi nzima ili kusajili wanachama wapya wa chama chao. Katika kipindi hicho kitakuwa na haki ya kufanya mikutano ya hadhara, lakini hakitakuwa na haki ya kushiriki au kuweka wagombea katika uchaguzi wowote. Kwa maana ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Uchaguzi Mkuu au Uchaguzi mdogo.

## 2. MAOMBI YA USAJILI KAMILI

Nyaraka za kuwasilisha wakati wa kuwasilisha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa maombi ya usajili kamili. Wanaoomba usajili kamili wa chama cha siasa watawasilisha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa nakala mbili ya Fomu PP.4 iliyojazwa kikamilifu. Fomu hiyo ipo katika Jedwali la Kwanza la Sheria ya Vyama vya Siasa. Maombi hayo yataambatana na nyaraka zifuatazo;

(a) tamko la kuthibitisha maombi katika Fomu PP.5 iliyowekwa kwenye Jedwali la Kwanza iliyojazwa kwa ukamilifu na kusainiwa na wanachama waanzilishi wawili wanaowasilisha maombi;

(b) nakala ya cheti cha usajili wa muda;

(c)Orodha ya wanachama wasiopungua mia mbili ambao wana sifa ya kuandikishwa kama wapiga kura kwa ajili ya uchaguzi wa wabunge kutoka angalau nusu ya mikoa ya Jamhuri ya Muungano ambayo kati yake angalau mikoa miwili iko Tanzania Zanzibar, ambapo mkoa mmoja kutoka Unguja na mkoa mwingine kutoka Pemba kwa kujaza Fomu PP.5A;

(d) maelezo ya kila mwanachama mwanzilishi katika PP.5C;

(e) maelezo ya viongozi wa kitaifa wa chama kwa kujaza Fomu PP.5B;

(e) uthibitisho wa malipo ya ada ya usajili kamili Shilingi milioni tano;